

HALMASHAURI YA MANISPAA TEMEKE

[Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa Temeke]

Simu: +255 22-292832
Fax: +255 22-2928137
Barua pepe: temeke@temekemc.go.tz
Tovuti: <http://www.temekemc.go.tz>



Ofisi ya Mkurugenzi
92 Barabara ya Mandele/Taifa
S.L.P: 46343,
15833 - DAR ES SALAAM,

Kumb Na. TMC/MD/A.5/45

Tarehe: 3/11/2017

NAFASI YA KAZI

Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke anawatangazia Wananchi/ Watanzania wote wenye sifa zinazotakiwa kuomba kujaza nafasi ya Mtendaji wa Mtaa daraja la III kwa sifa zifuatazo:-

AFISA MTENDAJI MTA A DARAJA LA III (Nafasi 5)

- **SIFA/ELIMU/UJUZI**
 - Elimu ya kidato cha Nnne (IV) , au Kidato cha Sita (VI,)
 - Cheti (Astashahada) cha Utawala, Sheria, Elimu ya jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya jamii na Sayansi kutoka Chuo cha Serikali ya Mitaa Hombolo Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

KAZI NA MAJUKUMU

- Katibu wa Kamati ya Mtaa.
- Mtendaji wa mtaa.
- Mratibu wa utekelezaji wa Sera na Sheria zinazotekelezwa na Halmashauri katika Mtaa
- Mshauri wa kamati ya Mtaa kuhusu Mipango ya Maendeleo ya katika Mtaa.
- Msimamizi wa utekelezaji wa Sheria Ndogo pamoja na sheria nyingine zinazotumika katika Mtaa
- Mshauri wa Kamati ya Mtaa kuhusu masuala ya Ulinzi na Usalama
- Msimamizi wa utekelezaji wa mikakati mbalimbali inayohusu uondoaji wa njaa na umasikini katika Mtaa
- Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na kutunza kumbukumbu za walipa kodi wote.
- Kuandaa na kutunza rejesta ya wakazi wote wa Mtaa na
- Atawajibika kwa Mtendaji wa kata.

NGAZI YA MSHAHARA

Ataanza mshahara **TGS B** kwa mujibu wa viwango vya Serikalini.

UMRI

Waombaji wote wanatakiwa wawe na umri usiopungua miaka **18** na usiozidi miaka **45**.

MAELEZO YA JUMLA

Maombi yote yawasilishwe yakiwa yameambatanishiwa na CV pamoja na nakala za vyeti vya kuhitimu elimu na mafunzo (vyeti vinavyoonyesha kiwango cha kufaulu na sio 'leaving certificate')

MUHIMU

Muombaji anatakiwa atume vyeti vyake halisi na halali kwani uhakiki utafanyika katika vyuo alivyopitia pamoja na Baraza la Mifihani. Udanganyifu wowote ukibainika hatua za kisheria zitachukuliwa.

MAOMBI YATUMWE KWA ANWANI IFUATAYO:-

MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE
S.L.P 46343
DAR ES SALAAM

Mwisho wa kupokea maombi ni siku ya Ijumaa tarehe **13/11/2017** saa **9.30 Alasiri**.

Imetolewa na,

NASSIB B. MMBAGGA
**MKURUGENZI WA MANISPAA
TEMEKE**